JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

# TAARIFA YA HALI MBAYA YA HEWA KWA MWEZI JANUARI NA FEBRUARI, 2024

## 1.0 UTANGULIZI

Katika kipindi cha miezi ya Januari na Februari, 2024 vipindi vya mvua viliendelea kujitokeza katika maeneo mengi ya nchi. Aidha, maeneo mengi yalipata mvua za juu ya wastani hadi wastani ikilinganishwa na wastani wa muda mrefu wa miezi ya Januari na Februari. Vipindi vya mvua kubwa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo. Hali hii ilisababisha mafuriko, ongezeko la unyevu ardhini na kina cha maji. Kwa upande mwingine, vipindi vya upepo mkali vilijitokeza katika maeneo machache ya ukanda wa Pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki. Hali ya hewa iliyojitokeza pamoja na athari zake imeendana na taarifa ya mwelekeo wa mvua za Msimu, 2023/2024.

### 1.1 Mvua kubwa kwa mwezi Januari, 2024

Katika kipindi cha mwezi Januari, 2024 vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo vilijitokeza katika maeneo mengi nchini. Aidha, maeneo mengi ya nchi yalipata mvua za juu ya wastani hadi wastani ikilinganishwa na wastani wa muda mrefu wa mwezi Januari. Vipindi vya mvua kubwa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini na kusababisha mafuriko, uharibifu wa miundombinu na mali, na hivyo kuathiri baadhi ya shughuli za kiuchumi. Mnamo tarehe 15 Januari, 2024 kituo cha Kilwa kilichopo mkoani Lindi kilipima milimita 186.5 za mvua kwa saa 24 ikiwa ni kiwango cha juu zaidi kwa mwezi Januari, 2024 ikifuatiwa na kituo cha Naliendele kilichopo mkoa wa Mtwara (milimita 113.3) na Tumbi kilichopo mkoa wa Tabora (milimita 112.2) mnamo tarehe 3 na 26 Januari, 2024 mtawalia. Jedwali 1 linaonyesha idadi ya siku ambazo vituo vilivyoripoti vipindi vya mvua kubwa vya milimita 50 au zaidi.

**Jedwali 1**. Idadi ya siku ambazo vipindi vya kubwa viliripotiwa vituoni kwa mwezi Januari, 2024

| Kanda | Kituo | Idadi ya siku | Mvua Kubwa (mm) |
|---|---|---|---|
| **Pwani ya Kaskazini** | Zanzibar | 1 | ≥ 50 |
| | JNIA (Dar es Salaam) | 2 | ≥ 50 |
| | Kibaha | 1 | ≥ 50 |
| | Morogoro | 5 | ≥ 50 |
| | Kizimbani | 1 | ≥ 50 |
| | Mlingano | 1 | ≥ 50 |
| | Ilonga | 1 | ≥ 50 |

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610


Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*728G _ 01/2023*

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Mahenge | 4 | ≥ 50 |
| **Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki** | Arusha | 1 | ≥ 50 |
| | Lyamungu | 1 | ≥ 50 |
| **Ukanda wa Ziwa Victoria** | Bukoba | 1 | ≥ 50 |
| | Ibadakuli | 1 | ≥ 50 |
| | Mwanza | 1 | ≥ 50 |
| | Ukiriguru | 1 | ≥ 50 |
| | Mwanza Marine | 1 | ≥ 50 |
| **Kati** | Hombolo | 1 | ≥ 50 |
| | Singida | 1 | ≥ 50 |
| **Magharibi** | Tabora | 2 | ≥ 50 |
| **Nyanda za Juu Kusini Magharibi** | Mbozi | 1 | ≥ 50 |
| | Iringa | 1 | ≥ 50 |
| | Songwe | 2 | ≥ 50 |
| | Igeri | 1 | ≥ 50 |
| **Pwani ya Kusini** | Kilwa | 1 | ≥ 50 |
| | Mtwara | 5 | ≥ 50 |
| | Naliendele | 5 | ≥ 50 |
| **Kusini** | Songea | 3 | ≥ 50 |

Katika kipindi cha mwezi Januari, 2024 ukanda wa pwani ulipata vipindi vingi vya mvua kubwa. Kituo cha Mtwara na Morogoro vilipata vipindi vya mvua kubwa vya milimita 50 au zaidi ndani ya saa 24 kwa siku tano. Aidha, vituo vilivyoripoti vipindi vya mvua kubwa vya milimita 70 au zaidi ndani ya saa 24 ni kama vinavyoonekana kwenye Kielelezo 1.




**Kielelezo 1:** Vituo vilivyoripoti viwango vya mvua kubwa kiasi cha milimita 70 au zaidi ndani ya saa 24 kwa mwezi Januari, 2024.


*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

Taarifa kutoka katika vyombo mbalimbali vya habari zilithibitisha kutokea kwa athari katika baadhi ya mikoa ikiwemo mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Morogoro, Lindi na Mtwara baada ya mvua kubwa kunyesha na kusababisha mafuriko, uharibifu wa mali na kuathiri baadhi ya shughuli za kiuchumi. Mnamo usiku wa tarehe 19 kuamkia 20 Januari, 2024 mvua kubwa iliyoambatana na upepo mkali ilisababisha uhabifu wa mali na miundombinu katika mkoa wa Dar es Salaam.



**Kielelezo 2**. Daraja linalounganisha Kunduchi na Bahari Beach likiwa limeharibika na kukatika baada ya mvua kubwa kunyesha (Chanzo: *Gazeti la Mwananchi*).

### 1.2 Hali joto kwa mwezi Januari, 2024

Katika kipindi cha mwezi Januari 2024, hali ya joto iliendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini. Aidha, hali ya joto zaidi ilijitokeza katika maeneo machache, hususan yale yaliyopo mwambao wa pwani. Kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 36.6 °C kilirekodiwa katika kituo cha Zanzibar kikifuatiwa na nyuzi 35.8 °C katika mkoa wa Dar es Salaam mnamo tarehe 19 Januari, 2024.


### 1.3 Upepo Mkali kwa mwezi Januari, 2024

Katika kipindi cha mwezi Januari, 2024 vipindi vya upepo mkali unaofika kilomita 40 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini ikiwemo ukanda wa pwani (Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba). Nguvu ya upepo ilisababisha athari mbalimbali ikiwemo kusambaa kwa vumbi, kupeperushwa kwa

takataka na kusababisha kupungua kwa uono. Maeneo machache ya mwambao wa pwani ya bahari yalipatwa na vipindi vya mawimbi makubwa na kuathiri baadhi ya shughuli zinazofanyika baharini sambamba na kuhatarisha jamii zinazofanya shughuli mbalimbali katika maeneo ya mwambao.

### 1.4 Mvua kubwa kwa mwezi Februari, 2024

Katika kipindi cha mwezi Februari, 2024 vipindi vya mvua vilijitokeza katika baadhi ya maeneo, hususan maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka. Aidha, vipindi vichache vya mvua kubwa vilijitokeza katika maeneo mbalimbali ya nchi. Mnamo tarehe 11 Februari, 2024 kituo cha Mahenge kilichopo mkoani Morogoro kilipima milimita 128.4 za mvua kwa saa 24 ikiwa ni kiwango cha juu zaidi kwa mwezi Februari, 2024. Vituo vilivyoripoti vipindi vya mvua kubwa vya milimita 50 au zaidi ni kama vinavyoonekana kwenye Kielelezo 3.




**Kielelezo 3:** Viwango vya mvua kubwa kwa mwezi Februari, 2024

### 1.5 Hali joto kwa mwezi Februari, 2024

Katika kipindi cha mwezi Februari 2024, hali ya joto ilijitokeza katika maeneo mengi ya nchi, hususan ukanda wa pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki. Kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 37.1 °C kilirikodiwa katika kituo cha Kilimanjaro (KIA) mnamo tarehe 18 Februari, 2024 ikiwa ni ongezeko la nyuzi joto 3.4 °C ikilinganishwa na wastani wa muda mrefu wa mwezi Februari. Aidha, hali ya joto ilijitokeza zaidi mkoa wa Kilimanjaro ambapo kwa siku 5 viwango vya joto la juu vilikuwa nyuzi joto 35 °C au zaidi.

**Jedwali 2**. Idadi ya siku ambazo viwango vikubwa vya joto la juu vilijitokeza kwa mwezi Februari, 2024

| Kanda | Kituo | Idadi ya siku | Kiwango cha Joto la Juu ($^0$C) |
|---|---|---|---|
| Nyanda za juu kaskazini mashariki | Kilimanjaro | 5 | ≥ 35 °C |
| | Moshi | 3 | ≥ 35 °C |
| | Same | 2 | ≥ 35 °C |
| Pwani ya Kaskazini | Tanga | 4 | ≥ 35 °C |
| | Zanzibar | 3 | ≥ 35 °C |
| | Dar | 1 | ≥ 35 °C |

**1.6 Upepo Mkali kwa mwezi Februari, 2024**

Katika kipindi cha mwezi Februari, 2024 vipindi vya upepo mkali unaofika kilomita 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini ikiwemo ukanda wa pwani (Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba). Aidha maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki pia yaliathiriwa na vipindi vya upepo mkali. Nguvu ya upepo mkali ilisababisha athari mbalimbali katika maeneo hayo.

*Matukio haya ya hali mbaya ya hewa yanaonesha ongezeko la changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na umuhimu wa kutekeleza mikakati thabiti ya kukabiliana mabadiliko hayo ili kulinda jamii na mazingira*.

*Imetolewa: tarehe 11 Machi, 2024*
**Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz